**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

# 687 VITENDO VYA KUJIFUNZA HAIBA NA MICHEZO

**Muda: Saa 3.** **Alhamis 14 Mei 2015 mchana**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka katika sehemu **B.**
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza kwa kifupi kanuni nne zinazopaswa kufuatwa na walimu wakati wa kuunda sheria za michezo na watoto.
2. Bainisha kwa kifupi namna nne ambazo mchezo wa kuigiza huimarisha uwezo wa kufikiri kwa watoto.
3. Onyesha mambo manne ambayo mwalimu anatakiwa kuepuka wakati wa kuchagua na kuandaa zana za kufundishia.
4. Kwa kutumia hoja nne eleza kwa kifupi umuhimu wa kuandaa uwanja au eneo maalum la michezo.
5. Fafanua kwa kifupi mbinu nne za majadiliano ambazo mwalimu anaweza kuzitumia kurekebisha tabia mbaya za watoto.
6. Eleza kwa kifupi dhana ya maendeleo kamili ya mtoto kama inavyohusishwa na Vitendo Vya Kujifunza Haiba na Michezo. Toa hoja nne.
7. Taja michezo minne ya ubunifu inayoweza kutumiwa kukuza ujasiri kwa watoto.
8. Eleza kwa kifupi umuhimu nne wa kutoa maelekezo mafupi na ya wazi kabla ya kuanza mchezo.
9. Bainisha aina nne za taarifa ambazo mwalimu anatakiwa kuziweka katika Kumbukumbu ya Matukio ya mtoto.
10. Eleza kwa kifupi faida nne za kutumia michezo ya ndani katika kipindi cha Vitendo Vya Kujifunza Haiba na Michezo.

## SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **manne (4)** katika sehemu hii

11. Kwa kutoa hoja tano jadili jinsi mwalimu anavyoweza kuwa kielelezo cha tabia njema kwa watoto wa Elimu ya Awali.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

12. Fafanua kwa kina aina tano za michezo ya ujenzi na ujengaji na umuhimu wake katika ukuaji wa mtoto.
13. Changanua kwa hoja tano athari za muda mrefu za kutumia lugha ya kuudhi au matusi kwa watoto wenye utovu wa nidhamu.
14. Eleza kwa kina mbinu tano anazoweza kutumia mwalimu ili kuendeleza utamaduni wa uwajibikaji kwa watoto katika michezo.
15. Onesha jinsi mazingira ya shule yanavyoweza kusaidia au kukwamisha jitihada za mwalimu za kufundisha nidhamu. Toa hoja tano.
16. Jadili kwa hoja tano dhana ya ujumuishi katika michezo na jinsi mwalimu anavyoweza kuitekeleza darasani.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org